

LEARNING BY EAR

“The Lost Kid – the Story of Single Mothers in Africa”

EPISODE 8: “Never say never again!”

AUTHOR: Mantegaftot Sileshi Siyoum

EDITOR: Stefanie Duckstein, Adrian Kriesch

PROOFREADER: Kate Hairsine

List of characters by scene:

SCENE ONE: DAY AT PAPA TILAHUN'S HOUSE

- **Papa Telahun (m, 76)**
- **Mama Beletu (f, 65)**
- **Kassech (f, 22)**
- **Begidu (m, 7)**
- **Narrator (m, around 35)**

SCENE TWO: NIGHT OUTSIDE THE LOCAL BAR

- **Mekete (m, 17)**
- **Challa (m, 16)**
- **Jonas (m, 15)**
- **Narrator (m, around 35)**

SCENE THREE: NIGHT OUTSIDE MR. MINABU'S COMPOUND

- **Drunkard Minabu (m,55)**
- **Papa Telahun (m, 76)**
- **Narrator (m, around 35)**

SCENE FOUR: NIGHT OUTSIDE MR. KASU'S COMPOUND

- **Mekete (m, 17)**
- **Challa (m, 16)**
- **Jonas (m, 15)**
- **Narrator (m, around 35)**

INTRO:

Hamjambo, wapendwa wasikilizaji! Huu ni mchezo wetu wa redio wa Noa Bongo Jenga Maisha Yako unaoitwa “MWANA MPOTEVU- KISA CHA KINA MAMA WANAOWALEA WATOTO WAO BILA BABA ZAO BARANI AFRIKA”. Katika sehemu iliyopita, Jonas nduguye mdogo Kassech pamoja na marifiki zake wawili, walikamilisha mipango ya kumuibia Bwana Kasu, ambaye ni tajiri sana katika eneo hilo. Wakati huo huo, Aster na babu na bibi yake walimpata Begidu, mwanawe Kassech, katika barabara ya mji mkuu akichokora pipa la taka kujitafutia chakula. Kumbuka, Begidu alitoroka kwa sababu ya mateso aliyokuwa akiyapata kwa mamake. Tegea sikio sehemu yetu ya nane iitwayo “HAYATATENDEKA TENA!” Kassech anaelekea nyumbani kwa wenye nyumba yake, Papa Tilahun na Mama Beletu. Wala hana habari kwamba mtoto wake amekwishapatikana.

SCENE ONE: DAY AT PAPA TILAHUN'S HOUSE

1. SFX: DAYTIME AMBIANCE FROM OUTSIDE, DOOR KNOCKED

2. Papa Tilahun: Alaa! Kassech, karibu ndani, mlango u wazi.

3. Kassech: Asante sana, Papa Tilahun.

KW Begin

4. Papa Tilahun: Kazi vipi?

5. Kassech Kazi inaendelea vyema, lakini samahani

sijalipa kodi mpaka sasa. Inshaallah nitakulipa kila kitu hivi karibuni.

6. Papa Tilahun: Ni sawa, tazama nafasi yako. Karibu ukae?

7. Kassech: **(Sits on the chair).**

8. SFX: CHAIR BEING PULLED

9. Papa Tilahun: Mara ya mwisho tulipoongea uliniambia ulikuwa na mpango wa kuanza tena masomo ya usiku.

10. Kassech: Ndiyo! Hiyo ndio sababu moja sijaweza kulipa kodo kwa wakati.

11. Papa Tilahun: Hilo la kodi lisikusumbue sana. Ninaelewa matatizo yako.

12. Kassech: Asante sana, Papa Tilahun! Mama Beletu aloponiambia unataka kuzungumza na mimi kwa dharura, nilidhani ni mambo ya kodi.

13. Papa Tilahun: **(Laughs)** Unadhani Papa Tilahun anazingatia tu kodi ya nyumba?

14. Kassech: Hapana, hapana, sisemi hivyo.

KW End

15. Papa Tilahun: Sawa! **(he laughs, and she laughs)** Una habari zozote kumhusu mwanao, Begidu?

16. **Kassech:** **(Very sadly)** Bado, Papa Tilahun, sijapata!
Ninajuta sana! Sikutenda lolote la sawa!
Nilidhani ni sawa kuwa mkali. Nilimtendea
Begidu, nilivyomtendea kwa kuwa mamangu
naye alinitendea vivyo hivyo. Sawa-yametokea
yaliyotokea.

17. **Papa Tilahun:** Unafahamu uliyoyatenda hayakuwa sawa.
Hivyo ni vizuri sana. **(Calls out)** Aster!
(Pause, someone appears).

18. **SFX: FOOTSTEP APPROACH**

19. **Kassech:** Shikamoo, Mama Beletu.

20. **Mama Beletu:** Marahaba, Kassech!

21. **Papa Tilahun:** Aster yu wapi?

22. **Mama Beletu:** Yeye na simu yake na simu yake na yeye. **(To Begidu)** Njoo, mwanangu.

23. **Begidu:** Mama! **(Runs)**

24. **Kassech:** **(Shocked)** Begidu!

25. **SFX: SOMEONE FALLS DOWN ON THE GROUND**

26. **Mama Beletu:** **(Frantically)** Ya rabi! Amepoteza fahamu!

27. **Begidu:** Mama! **(Cries)**

28. **Papa Tilahun:** Mbio! Mletee kikombe cha maji.

29. **Mama Beletu:** Yarabi! **(Runs to the other room).**

30. **Papa Tilahun:** Kassech, Kassech, Kassech!

31. **Begidu:** **(Cries).**

32. **NARRATION:** Kassech hajaamini aliyoyaona. Amepoteza fahamu. Siku hiyo hiyo baadaye, katika eneo hilo, Jonas, mdogo wake Kassech, anazungumza kwa uchangamfu pamoja na marafiki zake wanapoondoka kwenye baa. Si walevi ingawa wamekunywa pombe kiasi. Wako tayari kuvunja nyumba ya Bwana Kasu ambaye ndiye tajiri mkubwa sana katika eneo hilo.

SCENE TWO: NIGHT OUTSIDE THE LOCAL BAR

33. **SFX: WIND IS BLOWING, NIGHT AMBIANCE**

34. **SFX: THREE PEOPLE WALK ON A GRAVEL ROAD**

35. **Challa:** Siipendi baa ile, hasa wakati jirani yako mlevi Minabu akiwepo, Jonas.

36. **Jonas:** Sijui kwa nini leo hakunywa pombe nyingi kama ilivyo kawaida yake. Badala yake amekaa akitutumbulia macho.

37. **Mekete:** Msimtaje huyo mlevi. Nani ana kibiriti?

38. **Challa:** Hiki hapa! **(Fires the match).**

KW begin

39. **SFX: FIRING THE MATCH**

40. **Mekete:** Aisee! Unao ule msokoto?

41. **Challa:** **(Joking)** Msokoto?

42. **Jonas:** Ah, hebu acha masihara. Nipe mara moja.

43. **Mekete:** Challa! Una nini? Unajua fika, hivi punde tutakwenda kwa MTU TAJIRI ZAIDI HAPA MJINI.

44. **Challa:** Sawa , sawa! Pokeeni balaa yenu.

45. **Jonas:** Nipe!

46. **Mekete:** Hapana, navuta mimi kwanza!

47. **Challa:** Msiwe na wasiwasi, jamaa. Niliyo nayo inatutosha sote.

48. **Mekete:** Haya! Tuketini hapa- hakuna mtu hapa. **(They all sit)**

49. **SFX: DOG BARKING IN THE DISTANCE**

50. Mekete: Salala! Challa, mbona mbwa wako anapenda kutuandama kila mara hata wakati tuna shughuli muhimu kama leo? Unasubiri nini Challa?

51. Challa: **(Laughs)** Balaa, mbwa huyo huyo tena.

52. Jonas: **(Laughs)** Unataka kumpiga jiwe? Hili hapa.

53. Challa: Nipe.

54. SFX: DOG BARKING FROM DISTANCE FADEOUT

55. Challa: Anafhamu mambo kwa wepesi. **(They all laugh).**

56. Jonas: Ametoroka hata kabla yangu mimi kuinua mkono wangu.

57. Mekete: Sawa, naomba tena kibiriti.

KW end

58. SFX: FIRING MATCH

59. WIND IS BLOWING, THUNDERING

60. Mekete: Salala, huu upepo umezidi! Siwezi kuuwasha msokoto!

61. Jonas: Subiri! Nitakuingia upepo kwa mikono yangu.

(Pause)

62. SFX: FIRING MATCH

- 63. Mekete:** Naam! **(Inhales the marijuana deep and exhales)**. Shika! Ni zamu yako, Challa.
- 64. Challa:** Tujifurahishe kwa hii kwanza, ili usiku wa manane tutakapoamua kuruka ua wa yule bwana mambo yatakuwa mepesi. **(Inhales the marijuana deep and exhales)**.
- 65. Jonas:** Tuna kila kitu tunachohitaji?
- 66. Challa:** Chunguzeni orodha zenu! Acheni nijifurahishe na huu msokoto kwanza!
- 67. Jonas:** Nasema, je ulikumbuka habari ya nyama na sumu?
- 68. Challa:** Tayari! Sumu isikushughulishe. Niliifukia karibu na nyumbani kwa huyo tajiri.
- 69. Mekete:** Kwa nini ulifanya hivyo? Mbona hukuja nayo?
- 70. Challa:** Unasahau kwamba ni nyama yenye sumu? Afadhali hivyo nilivyofanya. Tukifika huko tutaifukua kisha tumrushie mbwa huyo. Si vizuri kubebana na sumu kila mahali. Ndiyo sababu nikafanya nilivyofanya!
- 71. Jonas:** Kweli!

72. Mekete: Naam! **(Smokes the joint)**. Si vizuri kubebana na vitu kama hivyo **(all laugh)**.

73. SFX: WINDS BLOWING, AND THUNDERING

74. NARRATION: Baadaye usiku huo, mlevi Minabu anarejea nyumbani. Anaishi jirani ya Kassech na Papa Tilahun. Ajabu kwamba Minabu leo hajalewa. Amekuja mbio kwa sababu ya mvua. Hasemi lolote. Minabu anapotafuta ufunguo mfukoni mwake, Papa Tilahun anatoka nje na kumwamkia. Anastaajabu kwamba mlevi leo hajalewa kitu wakati huu wa usiku kama ilivyo kawaida yake.

SCENE THREE: NIGHT OUTSIDE MR. MINABU'S COMPOUND

75. SFX: Night sounds, RAIN

76. SFX: CLINKING KEYS

77. Minabu: Pole! Papa Tilahun, sikuwa nimekuona, shikamoo!

78. Papa Tilahu: Marahaba, Minabu! Umerudi mapema leo.

79. Minabu: Naam, nimerudi mapema, Papa Tilahun.

80. Papa Tilahu: **(Hesitantly)** Mambo mazuri?

81. Minabu: Naam, mbona unaniuliza hivyo, Papa Tilahun?

- 82. Papa Tilahu:** Naona ajabu kwamba sauti yako haisikiki usiku huu kama kawaida yako!
- 83. Minabu:** Naam! Papa Tilahun, Nimeamua, "nimetosheka!" Na ninaamini unapokua na nia thabiti ya kubadilika, hakuna kinachoweza kukuzuia kubadilika.
- 84. Papa Tilahu:** Kweli, Minabu! Watu wengi huteseka kwa kuwa hawafahamu hivyo ulivyosema hivi punde.
- 85. Minabu:** Ndiyo, Papa Tilahun! Lakini kwangu mimi, huu ni uamuzi wa dhati!
- 86. Papa Tilahu:** Hayo ni matokeo ya dua zangu za kila asubuhi.
- 87. Minabu:** **(Laughs)** Asante sana, Papa Tilahun!
- 88. Papa Tilahu:** Si neno!
- 89. Minabu:** Nimegundua kuwa tabia yangu si mfano mzuri, hasa kwa vijana wa mji huu, kwa hivyo nikaamua kupunguza kiasi cha pombe ninayokunywa.
- 90. Papa Tilahu:** Kupunguza? Mbona usiache kabisa kunywa pombe?
- 91. Minabu:** Nitaacha siku za hivi karibuni.
- 92. Papa Tilahu:** Bora hivyo! Hoja ya maana ni hiyo nia yako ya kuacha pombe.

93. Minabu: Kwa hakika!

KW begin

94. Papa Tilahu: **(Speaks in low voice)** Umemuona jirani yako Kassech leo?

95. Minabu: Hapana! Kwani mwanawe ametoweka tena?

96. Papa Tilahu: Hapana, hajatoweka.

97. Minabu: Kwake hajawasha taa.

98. Papa Tilahu: Naam, nilimshauri ajipumzishe. Pengine ashalala.

99. Minabu: Sawa! Nimeelewa.

100. Papa Tilahu: Na wewe pia bora uzime taa kisha ujipumzishe.

101. Minabu: Nitafanya hivyo, Papa Tilahun, nimeupata ufunguo wangu.

102. SFX: CLINKING KEYS

KW end

103. Papa Tilahu: Lala salama!

104. Minabu: Na wewe pia!

105. SFX: DOOR BEING UNLOCKED AND OPEN

106. SFX: DOOR BEING CLOSED

107. SFX: DOOR BEING LOCKED

108. NARRATION: Minabu anakwenda kulala. Usiku umetulia isipokuwa sauti ya mvua inayomwagika. Hata hivyo kuna mambo ambayo hayaelekei kwenda sawa katika eneo hilo. Wale vijana watatu wamesimama katika ua wa nyumba ya Bwana Kasu. Wamepigwa na butwaa kwa mambo wanayoyashuhudia.

SCENE FOUR: NIGHT OUTSIDE MR. KASU'S COMPOUND

109. SFX: DOG BARKING INSIDE THE COMPOUND

110. SFX: ANOTHER DOG BARKING OUTSIDE THE COMPOUND

111. Challa: Mzuie huyo mbwa!

112. Jonas: Nini?

113. Mekete: **(In a low voice)** Nyamaza!

114. Challa: Balaa! Huyo mbwa mjinga ametimua mbio na nyama yenye sumu.

115. Mekete: Ulisema ulikuwa umeifukia ardhini!

116. **Challa:** Nilifanya hivyo lakini umemuona huyo mbwa akiifukua na kutoroka nayo.

117. **Jonas:** Tufanye nini sasa? Hatuna kipande kingine cha nyama ya kummaliza mbwa wa huyo tajiri!

118. **SFX: DOG BARKING INSIDE THE COMPOUND**

119. **Mekete:** **(In a low voice)** Tusipitie lango la mbele. Tuingilieni upande wa nyuma.

120. **SFX: THREE PEOPLE WALK ON A GRAVEL ROAD**

121. **SFX: DOG BARKING STOP**

OUTRO:

Na huo ndio mwisho wa sehemu ya nane ya mchezo wetu wa redio “MWANA MPOTEVU- KISA CHA KINA MAMA WANAOWALEA WATOTO WAO BILA BABA ZAO BARANI AFRIKA”. Bwana Kasu anaweza kuwa bado usingizini hata baada ya mbwa kubweka mfululizo? Nini kitakachomfika yeye na familia yake? Kwa mengi zaidi, jiunge nasi kwenye sehemu ijayo. Kumbuka, ukitaka kusikiliza sehemu hii tena au kuwasilisha maoni na mapendekezo yako fungua ukurasa wetu wa tovuti dw.de/lbe. Usikose kujiunga nasi katika sehemu ijayo- kwaheri!